# Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb
# Usajili wa Mtandaoni wa Shule ya Watoto
# Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara

## Wahusika wa Bahati Nasibu Mtandaoni wa Pre-k ya 2020-2021:

*Sehemu hii hutoa maelezo kwa wazazi/walezi ambao walishiriki katika mchakato wa bahati nasibu wa mtandaoni wa 2020-2021 na waliarifiwa kuwa watapata nafasi au kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri. Hakikisha umesoma sehemu ya mwisho yenye kichwa cha, Maelezo Muhimu ya Watu Wote.*

**Ninapaswa kufuata hatua zipi ikiwa mtoto wangu alipata nafasi katika bahati nasibu?**

Ikiwa mtoto wako alipata nafasi katika bahati nasibu, shule yako itawasiliana nawe baada ya muda mfupi. Shule inaweza kuhitaji hati kuwepo ikiwa haikuweza kusomeka au ilipitwa na wakati. Kwa kuongezea, shule itaomba kwamba hati zilizosalia zitumwe kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe. Orodha ya hati iliyosalia ilitumwa kwa wazazi/walezi wote baada ya bahati nasibu na kwa mara nyingine tena Juni 30, 2020 lakini inaweza kufikiwa kwa urahisi kwenye tovuti ya wilaya ya Pre-K katika: www.dekalbschoolsga.org/pre-k kwa ajili ya marejeleo.

**Ninapaswa kufuata hatua zipi ikiwa mtoto wangu aliwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri wakati wa mchakato bahati nasibu?**

Mwanafunzi yeyote ambaye hakuchaguliwa kwa nafasi ya bahati nasibu huwekwa kiotomatiki kwenye orodha ya wanaosubiri. Mfumo huo hupanga wanafunzi kinumerali kwenye orodha ya wanaosubiri. Barua pepe ilitumwa kumjulisha mzazi/mlezi kuhusu mpango wa mtoto kwenye orodha ya wanaosubiri. Kwa kuwa nafasi zinaweza kukataliwa au kubatilishwa, shule itajulisha familia inayofuata kwenye orodha ya wanaosubiri. Kwa wakati huo, utahitajika kukamilisha hatua zifuatazo ili kulinda nafasi ya mtoto wako. Shule itatambua mtu aliyechaguliwa wa usajili na kuwasiliana mzazi/mlezi kuhusu maagizo ya hati za kutumwa kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe.

## Waombaji Wapya Ambao Hawakushiriki katika Bahati Nasibu ya Mtandaoni ya Pre-K ya 2020-2021

*Sehemu hii hutoa maelezo kwa wazazi/walezi ambao hawakuweza kushiriki katika mchakato wa bahati nasibu wa mtandaoni wa 2020- 2021 na/au walituma maombi ya orodha ya wanaosubiri kwa shule ya karibu. Hakikisha kusoma sehemu ya mwisho yenye kichwa cha, Maelezo Muhimu ya Watu Wote.*

**Ninawezaje kuomba nafasi ya Pre-K kwa mtoto wangu ikiwa familia yangu haikushiriki katika bahati nasibu?**

Anza kwa kuwasiliana na shule ili kuona ikiwa kuna nafasi inayopatikana. Ikiwa kuna nafasi wazi, tafadhali endelea kujibu swali linalofuata. Ikiwa hawana nafasi inayopatikana, unakaribishwa kujaza maombi ya orodha ya wanaosubiri na kutuma kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe kwa mwakilishi wa usajili wa shule. Ikiwa huna uhakika wa ni nani ndiye mwakilishi wa usajili wa shule, tafadhali wasiliana na shule hiyo. Maombi ya orodha ya wanaosubiri inaweza kupatikana chini ya ukurasa, chini ya kichupo cha "Andikisha Sasa", kwenye tovuti ya Pre-K ya wilaya. www.dekalbschoolsga.org/pre-k.

**Ni hatua zipi zifuatazo za kujiandikisha kwa Pre-K ikiwa shule ina nafasi inayopatikana?**

Kamilisha mtandaoni Maombi ya Usajili wa Wanafunzi Mpya wa 2020-2021 kwa kubonyeza kiunga kinachofuatahttps://www.dekalbschoolsga.org/online-registration/new-students/.

**Ni nini hufanyika baada ya kukamilisha Maombi ya Usajili wa Mwanafunzi Mpya wa 2020-2021?**
Shule yako ya eneo lako itawasiliana nawe ili ushiriki maelezo yanayohusiana na hati ambazo zinahitajika kukamilisha mchakato wa usajili.

**Je, ni hati gani zinazohitajika kwa mwanafunzi kusajili katika Pre-K?**
Orodha kamili ya hati zote zinazohitajika inaweza kupatikana kwa kubofya kichupo cha "Mchakato wa Bahati Nasibu" kinachopatikana kwenye kiungo kinachofuata https://www.dekalbschoolsga.org/pre-k/.

## Maelezo Muhimu ya Watu Wote

**Na ikiwa siwezi kutoa Fomu 3231 ya Chanjo ya Afya kabla ya shule kuanza?**
Sera ya DCSD inasema kwamba ni lazima mtoto awe na fomu 3231 ya Chanjo ya Afya kwenye faili ndani ya siku 30 za mtoto kuanza shule au tarehe ya muda kuisha. Kwa sababu ya maradhi ya Covid-19, tafadhali tuma barua pepe kwa shule yako ukikumbana na matatizo ya kupata na kutuma hati hii kwa njia ya elektroniki. Wilaya itaendelea kufuatilia hali ya maradhi ya COVID-19 na kufanya maamuzi ya baadaye kulingana na mwongozo kutoka kwa Halmshauri ya Afya ya Jimbo la DeKalb, Vituo vya Udhibiti na Uzuizi wa Magonjwa, na Idara ya Afya ya Umma. Ikiwa fomu haijatolewa ndani ya siku 30 baada ya shule kufunguliwa, mtoto hataweza kurejea darasani bila fomu au uthibitisho wa miadi. Mtoto hataweza kurudi baada ya miadi bila fomu iliyosasishwa. Iwapo mtoto hatakuwa shuleni kwa siku 10 mtawalia kwa sababu ya fomu hii kutopeanwa, nafasi ya mtoto katika Pre-K itabatilishwa.

**Na ikiwa siwezi kutoa Fomu 3300 ya Kusikia, Kuona, Meno na Lishe kabla ya shule kuanza?** Sera ya DCSD inasema kwamba ni lazima mtoto awe na fomu kwenye faili ndani ya siku 90 za mtoto kuanza shule au tarehe ya muda kuisha. Kwa sababu ya maradhi ya Covid-19, tafadhali tuma barua pepe kwa shule yako ukikumbana na matatizo ya kupata na kutuma hati hii kwa njia ya elektroniki. Wilaya itaendelea kufuatilia hali ya maradhi ya COVID-19 na kufanya maamuzi ya baadaye kulingana na mwongozo kutoka kwa Halmshauri ya Afya ya Jimbo la DeKalb, Vituo vya Udhibiti na Uzuizi wa Magonjwa, na Idara ya Afya ya Umma. Ikiwa fomu haijatolewa ndani ya siku 30 baada ya shule kufunguliwa, mtoto hataweza kurejea darasani ambayo inaweza kusababisha mtoto kuondolewa kwenye mpango.

**Je, kuna sera ya mahudhurio kwa wanafunzi wa Pre-K?**
Ndiyo, kuna sera ya mahudhurio kwa wanafunzi wa Pre-K Kwa sababu ya COVID-19, marekebisho ya mahudhurio yameanzishwa. Wanafunzi wanatarajiwa kushiriki siku ya Pre-K ambayo ina maagizo ya saa 1 mtandaoni na kisha wakati uliosalia ni wa kukamilisha shughuli za nyumbani za kila siku zinazotolewa na mwalimu wa Pre-K. Siku ambazo somo halitafanyika, kwa sababu ya miadi au matukio mengine yasiyoonekana, somo la mtandaoni lililorekodiwa linaweza kutazamwa baadaye. Baada ya shule kufunguliwa tena, wanafunzi wanatarajiwa kuhudhuria siku nzima ya mafunzo katika kipindi cha mwaka mzima wa shule. Ikiwa mtoto hajahudhuria au amechelewa siku kumi mfululizo bila kisingizio cha matibabu, mtoto atatolewa darasani kulingana na miongozo iliyowekwa na Bright from the Start. Kwa kuongezea, mshauri na/au mhudumu wa jamii atawasiliana na wazazi/walezi ikiwa mtoto ana mfumo wa kuchelewa sana au kuondoka shule mapema.

**Je, kuna mahitaji yoyote ya kushiriki kwa wazazi/walezi wa Pre-K?**
Ndiyo, wazazi/walezi wanatarajiwa kushiriki katika mikutano na makongamano yote iliyopangwa ya mzazi/mlezi angalau mara mbili kwa mwaka na mara zaidi ikihitajika. Kwa sababu ya maradhi ya COVID-19, mikutano itafanyika mtandaoni. Mwalimu wa shule na/au mwalimu wa Pre-K atakuarifu wakati mkutano/kongamano utatokea na kutoa viungo vinavyofaa vya kujiunga na mkutano/kongamano ya mtandaoni. (Baada ya shule kufunguliwa tena, shughuli hizi zitadumu kwa takriban saa moja).

**Fafanua uzoefu wa kujifunza kwa mbali mtandaoni kwa wanafunzi wa Pre-K shule inapoanza.**
Wilaya itatoa hati ya wiki 4, shughuli za nyumbani kwa wanafunzi wote wa Pre-K ambazo zinaweza kukamilishwa bila kutumia teknolojia. Shughuli za nyumbani hutolewa kila baada ya wiki nne wakati wa mafunzo ya mtandaoni na kufuatilia Kujua Kusoma na Kuandika, Hisabati/Sayansi, Dhana ya Kijamii-Kihisia na Mwendo wa Jumla/Harakati ili kuchunguza na kujifunza. Mwalimu wa Pre-K atatoa kiungo cha mafunzo ambacho kinaweza kufikiwa kutoka kwa kifaa chochote cha kielektroniki.

**Itakuwa aje nikiwa na swali lolote ambalo halijashughulikiwa katika FAQ?**
Jihisi huru kuwasiliana na Ofisi ya Masomo ya Utotoni katika PreKRecords@dekalbschoolsga.org